BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kwanza – Tarehe 07 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 24 Juni, 2022.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa kufuta Sheria ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa), Nam. 4 ya 2007 na kutunga Sheria mpya ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa) katika kutekeleza kazi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa kufuta Sheria ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa), Nam. 4 ya 2007 na kutunga Sheria mpya ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa) katika kutekeleza kazi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

42. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF), kuna baadhi ya miradi haikamiliki vizuri na kukosekana kwa ufanisi wa miradi hiyo, kutokana na ukweli kuwa, fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi hiyo huwa ni kidogo ukilinganisha na ukubwa wa miradi husika.

Je, Serikali ina mkakati au mpango gani wa kuuongezea fedha mfuko huo ili uwendane na uhalisi wa maisha kwa wakati tulio nao sasa.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

59. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa mabadiliko ya tabia nchi (Climate Changes) yamesababisha upatikanaji wa mvua kuwa ndogo sana na hivyo kuongezeka kwa joto, jambo ambalo limepelekea uzalishaji wa mazao kuwa madogo sana. Na kwakuwa katika maeneo mbali mbali ya visiwa vyetu hivi viwili wananchi kwa kiasi kikubwa hupanda miti kama vile mivinje na mikarafuu inayofonza maji sana kwenye ardhi pamoja na vyanzo vya maji na hivyo kuzidisha ukame katika nchi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na changamoto hii.

(b) Je, Serikali imejipanga kuchukua hatua gani katika kukabiliana na changamoto hii.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

34. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Nane kwa kuongeza mishahara ya watumishi wa umma na kuanza kuilipa mishahara hiyo mipya mwezi wa Julai, 2022. Hata hivyo, kumejitokeza malalamiko kwa baadhi ya watumishi wa umma waliyoyawasilisha kufuatia tangazo la Katibu Mkuu wa Wizara yako la kuwataka wafanyakazi hao wajaze fomu maalum za malalamiko yao.

    Je, ni watumishi wangapi waliowasilisha malalamiko yao.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>**

39. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Miongoni mwa Sheria za wawekezaji Zanzibar ni pamoja na kujenga mahusiano mema na jamii inayowazunguka katika maeneo yao waliyoekeza, lakini pia kutakiwa kutoa kipaumbele katika nafasi za kazi (Ajira) kwa wananchi waliowazunguka. Kwa upande wa wananchi wa jimbo la Kiembesamaki, fursa hizo bado zimekuwa changamoto kuzipata.

    Je, Serikali kupitia Wizara husika ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa jimbo la Kiembesamaki kwa lengo la kuwawezesha kunufaika na fursa hizo ikiwemo ajira.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

1. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Katika mahabusu zetu nchini kumejitokeza changamoto kubwa ya kuongezeka kwa watuhumiwa jambo ambalo linahatarisha usalama na afya zao.

    (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza mrundikano wa mahabusu hao.

(b) Je, ni sababu gani zinazopelekea kurundikana kwa mahabusu hao katika vyuo vyetu vya mafunzo.

(c) Je, Wizara yako inatoa mchango gani wa kupatiwa dhamana mahabusu hao.

62. MHESHIMIWA MOHAMMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuanza hatua za awali za ujenzi wa soko katika jimbo la Mtambile za kusafisha na kukata mlima. Ni matumaini ya wananchi wa Mtambile azma hiyo ya Serikali itawaletea tija kubwa kibiashara.

(a) Je, ni lini Serikali itaanza rasmi kujenga soko hilo na lini linatarajiwa kumalizika.

(b) Je, ni aina gani za minada iliyopangwa kufanyika katika soko hilo.

(c) Je, Serikali inawahakikishia vipi wananchi wa jimbo la Mtambile kuhusu upatikanaji wa nafasi za kufanya biashara katika soko hilo.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

61. MHESHIMIWA MOHAMMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha wanafunzi wa Zanzibar wanasoma katika mazingira mazuri, wananchi wa jimbo la Mtambile wameamua kwa makusudi kujitolea kujenga skuli ya ghorofa itakayoondoa changamoto ya uhaba wa sehemu za kusomea jimboni mwao na maeneo yaliyopo jirani na jimbo lao.

(a) Je, Wizara itawasaidia vipi wananchi hao ili waweze kukamilisha ujenzi huo muhimu.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuisaidia skuli hiyo baada ya kukamilika ujenzi wake.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

36. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiwasomesha Mabwana Shamba na Mabibi Shamba ili kuwasaidia na kuwaendeleza wakulima katika shughuli zao mbali mbali za kilimo. Pamoja na kuwepo Mabwana na Mabibi Shamba hao, kumejitokeza tatizo la kutokuhamasishwa wakulima hao kulima kilimo cha alizeti ambacho kina faida sana kwao.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahamasisha wakulima kulima zao la alizeti ambalo mafuta yake yanatumika sana hapa nchini.

(b) Je, ni tani ngapi za mafuta ya kula zinaagizwa na kuingizwa hapa nchini.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

82. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na msongamano mkubwa wa magari kwa barabara ya Malindi hadi Bububu Polisi, hasa maeneo ya kwa Kisasi hadi skuli ya Bububu. Hali hii huleta kero kubwa kwa watumiaji wa barabara hiyo wakiwemo watalii.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulimaliza tatizo hilo.

(b) Katika mpango wa awali wa ujenzi wa barabara hiyo ya kwenda Mkoa wa Kaskazini Unguja, Serikali ilipanga kuijenga barabara hiyo kutoka Malindi mjini hadi Kinazini Mkwajuni Mkoa wa Kaskazini. Je, ni sababu zipi zilizopelekea ujenzi huo kuishia Bububu Polisi badala ya Malindi.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

3. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

   Imebainika kuwa kuwepo kwa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) kunapelekea wafanyabiashara kutozwa ada ya huduma husika mara mbili kwa jambo moja. Kitendo hiki kinawapa mzigo mkubwa wafanyabiashara hao.

   Je, Serikali ina mpango gani wa kuyaangalia tena majukumu ya Taasisi hizi kwa lengo la kuwaondoshea usumbufu wafanyabiashara wetu.

## IV. HOJA ZA SERIKALI

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.**

Mswada wa kufuta Sheria ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa), Nam. 4 ya 2007 na kutunga Sheria mpya ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa) katika kutekeleza kazi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**07 Septemba, 2022.** **KATIBU WA BARAZA.**